

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO

09 MEI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO – TAREHE 09 MEI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

207. MHESHIMIWA ESTER LUKAGO MIDIMU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wilaya za Itilima na

Busega ni Wilaya mpya na hazina Hospitali za Wilaya:-

Je, ni lini Serikali itajenga hospitali za Wilaya kwenye Wilaya hizo.

208. MHESHIMIWA RISALA SAID KABONGO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Vwawa ambayo inatoa huduma kwa Halmashauri nne za Mbozi, Ileje, Songwe na Momba inakabiliwa na upungufu wa vifaa tiba, wodi, Watumishi pamoja na Madaktari Bingwa:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupandisha hadhi Hospitali ya Vwawa kuwa Hospitali ya Mkoa ili iweze kutengewa bajeti ya kutosha kukabiliana na changamoto zilizopo sasa.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

209. MHESHIMIWA JOSEPHINE TABITHA CHAGULA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Kumekuwepo na tatizo kubwa la ukosefu wa maji safi na salama katika Mkoa wa

Geita pamoja na Wilaya zake kama Bukombe, Chato, Mbogwe na Nyang'hwale:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo hilo la maji kwa Wananchi wa Mkoa wa Geita na Wilaya zake.

WIZARA YA KILIMO:

210. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha inasambaza pembejeo kwa wakati na kwa kuzingatia msimu na jiografia ya maeneo husika.

211. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha Pamba yote iliyopo katika Jimbo la Bunda inanunuliwa kwa bei nzuri na kwa wakati muafaka;

(b) Katika Jimbo la Bunda kuna Kilimo cha Mkataba kwa kampuni moja na Wakulima wana hofu kuwa huenda kampuni hiyo isifanye vizuri kwa wingi wa Pamba iliyopo; Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya hali hiyo.

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

212. MHESHIMIWA OTHMAN OMAR HAJI (GANDO):

Atamuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Madhumuni makubwa ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) kilichoanza shughuli zake Julai 1978 kufuatia kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 ilikuwa ni kuendesha biashara ya Mikutano na upangishaji wa nyumba:-

Je, ni mafanikio gani ambayo Serikali imeyapata kutokana na kuanzishwa kwa Taasisi hiyo.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**213. MHESHIMIWA ENG. RAMO MATALA MAKANI
(TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Serikali inatekeleza Sera inayohusisha huduma bora za afya ya mama na mtoto:-

Je, utekelezaji huo umenufaishaje Jimbo la Tunduru Kaskazini.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**214. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Wilaya ya Mlele.

**215. MHESHIMIWA GIMBI DOTTO MASABA (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Itilima.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

216. MHESHIMIWA EDWIN MGANTE SANANDA (KONDOA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Je, ni lini Serikali itatekeleza Sera ya Elimu bure kwa kidato cha V na VI ambalo ndilo kundi pekee lililobaki

- kugharamiwa na Serikali.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
09 MEI, 2018**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**